02/2/2026

# TANGAZO LA KAZI (READVERTISEMENT)

## HOSPITALI YA WASSO – JIMBO KUU KATOLIKI ARUSHA

## WILAYA YA NGORONGORO

Hospitali ya Wasso inawatangazia Watanzania wote wenye sifa stahiki kuomba kazi katika nafasi ya Mhasibu, Mpishi Daraja la II, Muuguzi na Mkunga Daraja la II,Mtaalam wa Mionzi II, Tangazo hili ni readvertisement, hivyo waombaji waliotuma maombi hapo awali wanakaribishwa kuomba tena.

### 1. AFISA HESABU DARAJA LA II (ACCOUNTS OFFICER II) NAFASI (1)

#### a) SIFA ZA MWOMBAJI

- Awe na Shahada ya Uhasibu, Fedha, Uchumi au fani inayohusiana kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali
- CPA (T) au sifa nyingine inayolingana na kutambuliwa na Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi (NBAA) zitachukuliwa kama sifa ya ziada.
- Awe amesajiliwa na NBAA kama Certified public Accountant.
- Awe na ufahamu wa mifumo ya kifedha ya Serikali na Mifumo mingine ya Kiteknolojia ya uhasibu.
- Awe na uwezo mzuri wa kutumia kompyuta, hasa programu za uhasibu na MS Office (Word, Excel, Outlook).
- Awe na uzoefu au uelewa wa masuala ya fedha katika Sekta ya Afya.
- Awe na uwezo wa kufanya kazi kwa umakini, uadilifu, uaminifu na kwa kufuata taratibu za kifedha.
- Awe na mawasiliano mazuri, nidhamu, na uwezo wa kufanya kazi kwa kushirikiana na wengine.

#### b) MAJUKUMU YA KAZI

- Kuandaa na kutunza kumbukumbu za fedha za Hospitali kwa mujibu wa kanuni na taratibu.
- Kuhakikisha Mapato na Matumizi yote ya fedha yanarekodiwa ipasavyo kwenye mifumo ya uhasibu.
- Kuandaa hatimiliki, Vocha, Risiti, Malipo na nyaraka zote za kifedha.
- Kufanya upatanisho wa akaunti (Bank Reconciliation) kila mwezi.
- Kushiriki katika kuandaa bajeti ya mwaka, tathmini ya bajeti na taarifa za fedha za robo mwaka na mwaka mzima.
- Kuandaa na kuwasilisha taarifa za kifedha kwa uongozi wa Hospitali.
- Kufanya uhakiki wa madai kabla ya kufanyika kwa malipo.
- Kushiriki katika ukusanyaji na ufuatiliaji wa mapato ya Hospitali.
- Kuhakikisha uzingatiaji wa sera, sheria na kanuni za fedha za Serikali na Hospitali.

- Kushiriki katika Kufanya ukaguzi wa ndani na kusaidia ukaguzi wa nje unapohitajika,
- Kufanya majukumu mengine ya kifedha utakayopangiwa na mwajiri kulingana na taaluma yako.

2. **MPISHI DARAJA LA II (COOK GRADE II)** NAFASI (1)

**a) SIFA ZA MWOMBAJI**

- Awe na cheti cha kidato cha nne au kidato cha sita.
- Awe na Cheti cha Hotel Management kutoka chuo kinachotambulika na Serikali.
- Awe na uzoefu wa angalau miaka **miwili (2)** katika Hoteli, Lodge au hosteli ya kitalii.
- Uwezo wa kuandaa vyakula vya kimataifa (Continental & African dishes) utapewa kipaumbele.
- Awe na uelewa wa masuala ya **usafi wa chakula, huduma kwa wateja (Customer care), na usalama wa chakula (Food safety standards).**

  Awe na maadili mazuri, Mwaminifu, mchapakazi, na mwenye uwezo wa kufanya kazi kwa muda mrefu kulingana na ratiba ya wageni.

**b) MAJUKUMU YA KAZI**

- Kupika na kuandaa chakula bora kwa wageni na watalii wanaofikia katika Hospitali yetu kwa kuzingatia viwango vyenye ubora.
- Kuandaa menyu mbalimbali (Local & continental dishes) kulingana na mahitaji ya wageni.
- Kuhakikisha sehemu ya jikoni, vyombo na vifaa vya upishi vinakuwa safi muda wote.
- Kusimamia upokeaji, uhifadhi na matumizi sahihi ya malighafi za chakula.
- Kuhakikisha huduma za chakula zinatolewa kwa wakati, kwa usafi na kwa ukarimu.
- Kushirikiana na Uongozi katika kuboresha huduma na kuridhisha wateja.
- Kuhakikisha gharama za upishi zinadhibitiwa na kuzingatia bajeti ya mapato ya hostel.

3. **NURSE/MIDWIFE (MUUGUZI NA MKUNGA DARAJA LA II )** NAFASI (1)

**a) SIFA ZA MWOMBAJI**

- Awe na cheti cha kidato cha nne au kidato cha sita, Astashahada ((EN) Enrolled Nurse) na Stashahada ((ANO) Assistant Nursing Officer) ya Nursing and Midwifery kutoka chuo kinachotambulika na NACTE.
- Awe amesajiliwa na Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania (TNMC)
- Awe na leseni hai ya kufanya kazi (Valid Practicing license)
- Uzoefu wa kazi ya uuguzi katika mazingira ya vijijini utapewa kipaumbele
- Maadili mema, uwezo wa kufanya kazi kwa timu na kuhudumia kwa huruma.

**b) MAJUKUMU YA KAZI**

- Kutoa huduma za uuguzi kwa wagonjwa wa aina mbalimbali kwa kufuata miongozo ya kitabibu
- Kutoa huduma za Afya ya uzazi kwa wanawake wajawazito kabla na baada ya kujifungua.
- Kusimamia na kusaidia mama wakati wa leba na kujifungua kwa kuzingatia taratibu salama za kitabibu.
- Kufuatilia maendeleo ya Afya ya mama na mtoto mchanga baada ya kujifungua, na kutoa ushauri wa kitaalamu.
- Kutoa elimu ya Afya kwa wanawake kuhusu lishe , uzazi wa mpango , kunyonyesha , usafi wa mwili na mazingira.

4. **RADIOLOGY TECHNICIAN/RADIOGRAPHER (MTAALAMU WA MIONZI)**
   NAFASI (1)

   **a) SIFA ZA MWOMBAJI**

   - Awe na cheti cha kidato cha nne au kidato cha sita, Diploma ya Radiology/Medical Imaging kutoka chuo kinachotambulika
   - Awe amesajiliwa na Baraza la wataalamu wa mionzi Tanzania
   - Awe na leseni halali ya kazi
   - Awe na Ujuzi wa kutumia mashine za digital X-ray, Utrasound
   - Awe na Uwezo wa kufanya kazi kwa kujitegemea na kwa kufuata maadili ya kazi.

   **b) MAJUKUMU YA KAZI**

   - Kuchukua picha za ndani ya mwili wa binadamu kwa kutumia mionzi (kama X-ray).
   - Kumwandaa na kumuelekeza mgonjwa kabla na wakati wa upigaji wa picha
   - Kuhakikisha usalama wa mgonjwa dhidi ya madhara ya mionzi kwa kutumia vifaa vya kujikinga na kudhibiti kiasi cha mionzi kinachotumika.
   - Kuendesha na kudhibiti vifaa vya mionzi ili kuhakikisha vinafanya kazi kwa usahihi.
   - Kuhifadhi na kuwasilisha picha na taarifa za uchunguzi kwa wataalamu husika.
   - Kudumisha usiri na heshima kwa wagonjwa.

**MASHARITI YA JUMLA**

i. Mwombaji awe ni Raia wa Tanzania na mwenye umri usiozidi miaka 45.
ii. Cheti cha mtihani wa kidato cha IV na VI.
iii. Mwombaji aambatishe nakala ya cheti cha kuzaliwa, Kitambulisho cha Taifa (NIDA) au kitambulisho cha mpiga kura.
iv. Mwombaji aambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (Referees) watatu wa kuaminika.
v. **Testimonials, Provisional Results, Statement of Results, hati ya matokeo ya kidado cha nne na sita (FORM IV AND VI RESULTS SLIPS) HAVITAKUBALIWA.**
vi. **Mwombaji aliyesoma nje ya Tanzania ahakikishe cheti chake kimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (TCU au NECTA).**
vii. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi mhusika atachukuliwa hatua za kisheria.
viii. **Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe 15 February, 2026.**
ix. **Maombi yawasilishwe kwa njia ya barua kwa Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Wasso S. L.P. 42, LOLIONDO, barua pepe. secretary@wassohospital.org.**

WASSO HOSPITAL P.O. BOX 42 LOLIONDO ARCHDIOCESE OF ARUSHA

........................

Angela Joseph
**Kny: MGANGA MFAWIDHI**